

# TUMRUDIE MUNGU

---

Hiki ni kitabu kinachoonyesha jinsi mungu alivyo katika maisha yetu ya kila siku katika mazingira yetu haijarishi unakutana na magumu kiasi gani Ila mungu bado yunasi,

Na kamwe hatuachi matatizo na changamoto zinaweza kukufanya uhisi mungu hayuko nawewe sio kweli yeye yuko nawewe na hatokuacha.

Mwandishi: PHABIAN ISAYA

---

Shukrani

Kwanza namshukuru mungu kwakuniwezesha kupata hekima yakuweza kuandika kitabu hiki shukrani kwa wafuatao,

Padre Benedict Magabe, Padre Thadeus Memba, Padre Faustine Kamugisha, Advocate Vedastus Laurean, Dr Ernesta Masha (mkurugenzi idara ya Kiswahili chuo kikuu cha udsu), Profesa Willam Nangiyse (mkuu wa chuo kikuu cha dare s slaam),

Sister Theresia Swai, Familia yangu Jumuiya ya mt Bakita dar es slaam, chama cha kitume cha Legio Marie parokia ya Mt Gaspal De Bufallo (Dar es slaam).

## **SURA YA KWANZA**

### **JE MUNGU YUPO KATIKA MAISHA YAKO YA KILA SIKU?**

Maisha yana maana nzuri kama utatambuwa uwepo wa mungu katika maisha yako ukiweza kulifahamu hilo linaweza kuwa fanikio namba moja kwenye maisha yako ya kila siku.

Ilikuweza kujridhisha kama uko na mungu jiulize umepitia mangapi magumu? Yawezekana uko kwenye mpito wa shida hiyo haimaanishi mungu hatendi matendo makuu kwako,

wanadamu wengi wanapoingiwa na tatizo flani wanahisi labda mungu amewaacha ndiyo maana kuna kuwa na mkorogano wa maswali ambao unaweza kuupata kipindi unakabiliwa na matatizo mengi.

Mungu uko wapi? Au mungu yupo kweli? Yawezekana ndiyo maswali hapo ulipo au unapokuwa katika nyakati ngumu zinazoweza hata kulegeza imani yako. Ukweli kuhusu mwanadamu wa karne ya 21 ametawaliwa na hisia ambazo zinampelekea kushindwa kuelewa ukuu wa mungu katika vitu vingi watu wanaweza kutoa shuhuda nyingi lakini kuna ushuhuda mzito huwa wana usahau,

Matendo makuu ya mungu katika uhai unaweza kuwa moja ya shuhuda nzuri ukiwa na afya nzuri huna tatizo linalokusumbua kiafya shukuru mungu kwakuwa afya ni bora zaidi kuliko vitu unavyohitaji.

Uhai wa mwanadamu ni moja ya fadhira za mungu jiulize kama una magonjwa utawezaje hata kusimama? utawezaje kuomba utawezaje kuimba n.k.

Hivyo vyote vinafanyika endapo utakuwa na zawadi ya uhai mungu aliyokutunukia kila unapoamka mshukuru mungu kwa uhai ulionao ni moja ya jambo kubwa katika matendo makuu ya mungu,